

# Sababu za kukwama kwa sekta ya viwanda (1)

Viwanda vya sukari nchini ni moja ya sekta iliyofanikiwa kidogo ukilinganisha na viwanda vingine Tanzania. Picha ya Maktaba.

**Taasisi za fedha zinazojua kazi zake zinapeleka mapato wanayokusanya kwenye sekta za uzalishaji**

Veneranda Sumila,Mwananchi

Mpango wa kubadili Mji wa Arusha kuwa mji wa watu wenye kipato cha kati na kulisha Tanzania na nchi jirani ya Kenya, umeyeyuka baada ya kuwapo kwa mazingira ambayo si rafiki kwa biashara.

Kwa miongo miwili sasa, sekta ya viwanda mkoani Arusha na Tanzania kwa ujumla imekuwa ikiporomoka kutokana na sababu mbalimbali.

Utafiti uliofanywa na Shirikisho la Biashara, wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA-Arusha), umebainisha kwamba kuanguka kwa sekta hiyo kumesababishwa na mambo mengi.

Taarifa ya utafiti huo imebainisha kwamba mafanikio ya sekta ya viwanda yanategemea sana mazingira yanayosimamia upatikanaji wa teknolojia na matumizi yake.

**Matatizo ya kiutawala**

Matatizo ya kiutawala yaliyopo katika sekta za umma nchini Tanzania, yamesababisha sekta ya viwanda kushindwa kujiendesha kiushindani.

Kwa mujibu wa shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu (Unesco), viwanda vingi vinaendeshwa kwa hasara kutokana na kuwapo kwa gharama kubwa za uzalishaji, tija ndogo, riba kubwa za kibenki na ugumu katika sheria za kubadilisha fedha za kigeni.

Pia Kamisheni ya Unesco nchini Tanzania, imetaka kuwapo na ushindani kwa kuzingatia sera za biashara huru.

Taarifa ya utafiti huo zinaonyesha kwamba shughuli zinazoendeshwa na taasisi nyingi zinakabiliwa na urasimu mkubwa, rushwa, na kutokuwapo kwa ukweli katika mikataba ya umma.

Utafiti huo ulifanywa na (TCCIA) mkoani Arusha kwa kufadhiliwa na BEST-AC na kubainisha kwamba vikwazo vinasababisha kuwapo kwa gharama zisizokuwa za lazima katika shughuli za uzalishaji viwandani na kupunguza kasi katika mchakato wa maendeleo.

Mazingira ya kiuchumi pia ni kikwazo cha maendeleo ya viwanda nchini.

Kutokana na utafiti huo, madeni ya serikali ya nje na ndani, yana athari katika sekta ya viwanda katika kuleta maendeleo ya viwanda.

Kazi ya kulipa madeni ya serikali kunazuia uwezo wa serikali kuwekeza katika viwanda kwa kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha uwezo wa viwanda hivyo kiuchumi.

"Mfumuko wa bei unakwamisha maendeleo ya viwanda. Na mafaniko ya viwanda yanategemea zaidi makisio sahihi ya gharama za uzalishaji," inasema ripoti hiyo.

Changamoto nyingine zinazokwamisha maendeleo ya viwanda ni elimu.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo Tanzania ipo katika matatizo makubwa ya ubora hasa katika elimu yake ya msingi.

"Wengi wa wafanyakazi katika sekta ya viwanda ni wa darasa la saba (elimu ya msingi), lakini cha ajabu wengi wa wanaomaliza elimu hawajui kusoma wala kuandika," inasema ripoti hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti huo, elimu ya msingi ya Tanzania hivi sasa ipo katika hali mbaya kiasi ya kwamba ni vigumu kuwaendeleza ili wamudu teknolojia mpya za viwandani.

Kutokana na hali hiyo ni ukweli usiopingika kwamba wanafunzi wengi waliomaliza elimu ya msingi wanaweza kufanyakazi nyepesi tu, wengi wanashindwa kufanya kazi zenye teknolojia ya hali ya juu.

Wanafunzi wenye elimu ndogo au msingi wanakuwa na ubunifu mdogo sana katika mlolongo wa uzalishaji mali. Kwa msingi wa tatizo hilo ni vigumu sana kwa viwanda kuingiza teknolojia ya kisasa ili kuongeza ubora na tija kutokana na kukosekana kwa raslimali watu yenye uwezo wa kwenda sambamba na teknolojia mpya.

"Ni muhimu sana kwa serikali ya Tanzania kuachana na mawazo ya kupunguza fedha ya kwenye sekta ya elimu kwa sababu ni eneo muhimu kwa maendeleo ya nchi," inasema sehemu ya ripoti hiyo.

Jambo lingine ambalo limekuwa likikwamisha sekta ya viwanda kukua ni soko la fedha.

**Viwanda vidogo ni muhimu**

Kwa mujibu wa taarifa hiyo taasisi za fedha zinafanya juhudi kubwa ya kukusanya fedha. lakini wanakuwa wazito kuwekeza katika maeneo muhimu ya uchumi kama viwanda vidogo na vya kati.

"Taasisi ya fedha inayojua kazi yake inapeleka fedha zilizokusanywa katika sekta za uzalishaji," inasema sehemu ya ripoti hiyo.

Ongezeko la tija katika historia ya dunia kunatokana na binadamu kufanikiwa kukua kiteknolojia. Mbali na hayo kubadilika kwa teknolojia kunawezeshwa na mazingira bora ya ubunifu kwa ufadhili wa sekta binafsi na umma.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo kunatakiwa ushirikiano wa kutosha katika utafiti na maendeleo ya teknolojia kati ya vyuo vikuu na sekta ya viwanda. Mambo mengi hivi sasa hayafanikiwi kutokana na njia zisizosahihi zinazotumika kufanya utafiti na kuupeleka kwa watumiaji.

Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi wa simu kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe

**Usikose kusoma sehemu ya pili ya makala haya wiki ijayo.**

**HABARI ZAIDI**

- Kanuni za kuwezesha maendeleo ya viwanda ni dhaifu.
- Tabia za maofisa wa umma, hasa mawazo yao finyu kuhusu sekta binafsi kunawachosha wajasirimali.
- Kukinzana kwa kanuni na tozo kubwa ni kikwazo kingine kwa maendeleo kwa wajasiriamali.
- Kukosekana kwa miradi ya EPZ na SIPZ mkoani kunasababisha wajasiriamali kufanya kazi moja na kukosa ushindani ambao ni muhimu.
- Viwango vya elimu na uelewa unazuia kukua kwa teknolojia na ubunifu katika sekta ya viwanda

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI